
Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

TaTEDO

MTANDAO WA JAMII WA USIMAMIZI WA MISITU TANZANIA
MJUMITA

Schweizerische Eidgenossenschaft
Confédération suisse
Confederazione Svizzera
Confederaziun svizra

# Taratibu za kuhusisha uzalishaji endelevu wa mkaa katika Usimamizi wa Misitu ya Jamii



2015



Kiongozi hiki kimetayarishwa kwa msada toka Shirika la Maendeleo na Ushirikiano la Uswisi (Swiss Agency for Development and Cooperation) kama sehemu ya Mradi wa Kuleta Mageuzi katika Sekta ya Mkaa Tanzania.

**Kimetolewa na:**

Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG),
S.L.P. 23410, Dar - es – Salaam,
Tanzania.

Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA),
S.L P 21522, Dar es Salaam,
Tanzania.

Shirika la Kuendeleza Nishati Asilia Tanzania (TaTEDO), S.L.P 32794
Dar es Salaam,
Tanzania.

**Michoro na Usanifu na:**
Athman Mgumia,
S.L.P 4011, Morogoro,
Tanzania.

Mobile Simu: 0754 687067/ 0786 118295

© Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

# Taratibu za kuhusisha uzalishaji endelevu wa mkaa katika Usimamizi wa Misitu ya Jamii



**2015**



## YALIYOMO


1. Utangulizi ........................................................................ 1
2. Ujumbe kuhusu umuhimu wa usimamizi endelevu wa misitu........................................................ 2
3. Maeneo ya Uvinaji wa miti kwa ajili ya mkaa............... 3
4. Mipaka ya Uvunaji ............................................................ 6
5. Miti ya mbao inayopaswa kuvunwa ............................... 10
6. Rangi za kuwekea Alama miti......................................... 10
7. Hatua za Uvunaji ............................................................... 12
8. Kuweka Kumbukumbu za takwimu ................................ 13

## 1. Utangulizi

Kiongozi hiki cha uvunaji wa mkaa kilitengenezwa kama sehemu ya Mradi wa Kuleta Mageuzi katika sekta ya mkaa Tanzania, mradi wa ubia kati ya Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo na Ushirikiano la Uswisi (SDC). Kiongozi hiki kimeandaliwa ili kusaidia Kamati za Maliasili za vijiji kupanga uvunaji wa mkaa katika misitu ya hifadhi ya vijiji iliyotengwa kwa ajili ya shughuli hiyo. Kiongozi hiki kinakusudia kuweka mlinganisho kati ya hitaji la haraka la kukata miti kwa ajili ya kutengeneza mkaa na hitaji kubwa zaidi la kuendeleza ikolojia na uwezo wa uchipuaji wa misitu ya miombo.

Kiongozi hiki cha uvunaji kinafaa zaidi kwa ajili ya usimamizi wa misitu  ya miombo yenye unyevu mwingi na inatokana na kuamini ya kwamba:

Kulingana na Frost (1996), katika misitu  ya miombo yenye unyevu mwingi, kiwango cha ukuaji mwanzoni ni cha kasi zaidi na kupungua kadri muda unavyo kwenda. Ukuaji wa juu zaidi unaonekana kwa miaka ya 18 na kiwango cha ukuaji wa wastani kinapungua baada ya miaka 24. Kiwango cha wastani kwa mwaka cha ukuaji wa miti katika misitu  ya miombo yenye unyevu mwingi kwa miaka 24 ya kwanza ni miligramu  2.8 kwa hekta. Hivyo, ndani ya miaka 24, kama miti ya miombo iliyokomaa inaanza na miligramu  90 kwa hekta ya ujazo wa miti kabla ya kuvunwa, ndani ya miaka 24, asilimia 75 ya miti itachipua upya (kama miti yote ya mwanzo ilikatwa, lakini katika hali halisi misitu michache zaidi ya 100% ya miti yote itakatwa

Wakati ujuzi wetu wa misitu yenye unyevu mwingi ya miombo unaboreshwa, tunaweza kupata muda mzuri zaidi wa mzunguko kwa ajili ya uzalishaji wa mkaa, ambao unaweza kuwa zaidi au chini ya miaka 24.Kwa sababu hiyo, sehemu ya kwanza iliyotengwa kwa ajili ya uvunaji wa mkaa inapaswa kuwa si zaidi ya asilimia 25 ya eneo lote la msitu wa kijiji, ili muda wa mzunguko uweze kuongezwa kama inahitajika kwa kuongeza ukubwa wa eneo la uvunaji wa mkaa katika siku za usoni..





Miti ya Miombo ni aina ya miti inayohitaji mwanga sana na inakuwa haraka sana ikiwa na mwanga mwingi wa wazi. Hivyo, uvunaji wa kuchagua sana wa miti katika misitu iliyofunga matawi sana utapelekea ukuaji wa taratibu kuliko uvunaji wa kutochagua sana, hasa kama uvunaji wa kuchagua unaacha visiki ambavyo vinaweza kuchipua au kuotesha mizizi katika vivuli kwa muda mwingi wakati wa mchana. Eneo la mita 50 kwa 50 lililovunwa litatoa mwanga wa kutosha kwa ajili ya uchipuaji kwa sababu vipimo vyake ni karibu mara mbili ya urefu wa miti ya miombo iliyokomaa. Kwa hiyo, maeneo yote yaliyovunywa kwa upana wa mita 50 kwa 50 yatapata mwanga wa jua moja kwa moja kwa kipindi fulani kwa siku.

Hata hivyo, ufyekaji wa miti yote kwa pamoja pia haushauriwi kwa sababu unaweza kusababisha mabadiliko ya kimazingira ambayo yatahamasisha ukuaji wa nyasi zaidi, ambayo itapelekea mioto ya mara kwa mara au joto kali. Pia kwa kuondoa miti yote kwa mara moja kwenye miteremko kunaweza kusababisha mmomonyoko wa udongo. Kwa hiyo, mapendekezo yafuatayo yanalenga kuhakikisha kwamba uvunaji wa miti kwa ajili ya mkaa haupelekei ufyekaji wa maeneo makubwa sana, kwamba baadhi ya miti inaachwa katika maeneo yaliyopangwa kuvunwa, na kwamba ukuaji unaofaaumetokea kabla ya uvunaji mwingine kuendelea katika maeneo yaliyo jirani.

## 2. Ujumbe kuhusu umuhimu wa usimamizi endelevu wa misitu

Uzalishaji endelevu wa mkaa na uhifadhi wa misitu una manufaa makubwa kwa watu ikiwa ni pamoja na kuzalisha chakula, nishati ya mafuta, mijengo na dawa za asili.
Msitu pia unazuia mmomonyoko wa udongo, vyanzo vya maji, hewa safi, pia inasaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na kuhifadhi baioanuwai.

Uvunaji endelevu wa mkaa vilevile huwezesha kupatikana kwa fedha za kusaidia vijiji kulinda misitu yao ya hifadhi. Kama misitu italindwa kama inavyo takiwa, miti iliyovunwa inaweza kuchipua

upya na kufanya vijiji kuendelea kunufaika na mazao ya misitu. Mafanikio haya yanaweze kufikiwa iwapo kila mtu atafuata sheria ndogo za vijiji na kutekeleza mpango wa matumizi endelevu ya misitu.

Fuata sheria ndogo za kijiiji chako usaidia kuhifadhi msitu wako.

## 3. Maeneo ya uvunaji wa miti kwa ajili ya mkaa

Hatua ya kwanza wakati wa kupangilia uvunaji wa mkaa katika msitu wa hifadhi wa kijiji ni kuchagua na kuweka alama katika maeneo ya misitu ya hifadhi ya msitu wa kijiji kama maeneo ya usimamizi wa misitu kwa ajili ya uzalishaji wa mkaa. Maeneo haya yanapaswa kuwa yanafikika na wanajamii na yasiwe mbali sana na barabara. Inaweza kuwa ni vyema kuangalia maeneo ambapo watu walikuwa wanavuna mkaa zamani kabla hifadhi ya msitu wa kijiji haujatengwa. Eneo hili lisijumuishe miteremko mikali, migongo ya vilima virefu vilivyoinuka au maeneo ambayo wakati mwingine yanakuwa na nyasi ndefu sana. Ni muhimu sana kuepuka maeneo kama haya kwa sababu yanatabia ya kuwa na mioto mikali sana ambayo itafanya uchipuaji baada ya kuvuna miti kuwa mgumu sana. Afisa Misitu wa Wilaya na wataalamu wa misitu katika vyama vya kiraia wanaweza kusaidia wanakijiji kuchagua eneo bora. Pale ambapo eneo limesha ainishwa, Mkutano Mkuu wa Kijiji unapaswa kupitisha matumizi ya eneo dogo la usimamizi wa msitu kwa ajili ya uzalishaji wa mkaa endelevu.

Uvunaji wa miti kwa ajili ya mkaa kwenye misitu ya hifadhi ya kijiji unapaswa kufanyika katika maeneo ya usimamizi yaliyotengwa kwa ajili ya uzalishaji wa mkaa kama ilivyo ainishwa bayana kwenye Mpango wa Usimamizi wa Msitu. Na jumla ya maeneo ya yaliyotengwa kwa ajili ya usimamizi hayapaswi kuwa zaidi ya asilimia 20 ya eneo lote la msitu wa hifadhi ya kijiji kwa miaka 24 ya kwanza. (Hii ni kwa ajili ya kuruhusu muda wa mzunguko kama inahitajika). Eneo dogo la usimamizi litagawanywa tena katika maeneo madogo ya usimamizi ya mita 50 kwa 50. Maeneo haya yanaitwa vitalu. Vitalu hivi vitarahisisha kupanga uvunjaji



wa mkaa na mbao ambao uko katika vitalu hivi, ili kuhakikisha kwamba maeneo madogo ya usimamizi hayatavunwa zaidi, na kuhakikisha kwamba uvunaji hausababishi mmomonyoko wa udongo.


Kila mwaka, Kamati ya Malisili ya Kijiji itaweka alama kwenye idadi maalumu ya maeneo ya upana wa mita 50 kwa 50 ya vitalu vitakavyovunwa kwa kutumia ramani ya vitalu vyote. Kila kitalu kina nambari ya kipekee kwenye ramani na ramani pia itaonyesha tarakimu za GPS za pembe zote za vitalu. Ramani pia itaainisha idadi ya juu ya vitalu ambavyo vinaweza kuvunwa kwa mwaka, ambayo itakuwa sawa na jumla ya idadi ya vitalu katika eneo dogo la usimamizi wa misitu lililogawanywa katika vipande 24.

Kama kuna sehemu ya eneo dogo la usimamizi wa msitu imekatwa na haikupaswa kukatwa kulingana na mpango, hapo Kamati ya Maliasili ya Kijiji inapaswa kuhesabu idadi ya vitalu vilivyo athirika na ukataji huo na kutoa kiasi hicho kutoka kwenye jumla ya idadi ya vitalu vinavyopaswa kuvunwa kwa mwaka huo. La sivyo, kijiji kitakuwa kinavuna eneo hilo kwa kiwango ambacho siyo endelevu.


Kila mwaka, Kamati ya Maliasili ya Kijiji inapaswa kujadiliana na wachoma mkaa kabla ya kuweka alama kwenye vitalu vya mita 50 kwa 50 vitakavyovunwa ili kuhakikisha kwamba wachoma mkaa kutoka maeneo mbalimbali ya kijiji wanaweza kufikia na kutumia vitalu hivyo. Mathalani, kama kuna maeneo mengi ya usimamizi katika msitu wa hifadhi wa kijiji, lakini kamati ikawekea alama vitalu vilivyoko katika eneo moja tu la usimamizi wa misitu upande wa kusini mwa kijiji, watu kutoka upande wa kaskazini mwa kijiji wanaweza kupata ugumu wa kutengeneza mkaa kwa kufuata sheria na taratibu.

Ili kuzuia mmomonyoko wa udongo unaosababishwa na uvunaji, vitalu ambavyo vinapaswa kuwekewa alama kwa ajili ya kuvunwa kwa mwaka husika havipaswi kupakana kabisa

lakini vinakuwa kwa mustazali (angalia mchoro 1). Vitalu ambavyo havijavunwa na viko karibu na vitalu ambavyo vimeshavunwa havipaswi kuchaguliwa kwa ajili ya kuvunwa hadi hapo vitalu ambavyo vilishavunwa vimeoteana na kukomaa kwa angalau




*Mchoro 1: Uvunaji wa miti ya kutegeneza mkaa utafuata vitalu vilivyoko mkabala kama mishale inakoelekeza ili kuzuia mmomonyoko wa ardhi*




*Mchoro 2: Vitalu vilivyo baki vitaanza kuvunwa baada ya zaidi ya miaka kumi (10) kuruhusu vitalu vilivyovunwa kuchipua na kuwa na uwezo wa kuzuia mmomonyoko wa adhi*






miaka 10 (angalia mchoro 2). Hii itahakikisha kwamba vitalu vilivyovunwa vina uoto mzuri na vina mizizi inayoendelea vizuri ambayo itazuia mmomonyoko wa udongo kabla vitalu vya jirani havijaanza kuvunwa.
Ili kuwarahisishia wachoma mkaa kuona mipaka ya vitalu ambavyo vinavunwa, pembe zote za vitalu vitakavyovunwa vinapaswa kuwekewa alama. Mjumbe wa Kamati ya Maliasili ya Kijiji anapaswa kutumia kifaa cha GPS kupata pembe ya kitalu cha kuvuna na kuweka alama kwenye mti ulioko karibu zaidi (angalia mchoro wa kuweka alama ya miti iliyoko kwenye pembe). Kama hakuna mti ndani ya mita tatu ya pembe ya kitalu mjumbe wa Kamati ya Maliasili anapaswa kukata mrunda/nguzo, auwekee alama kulingana na mwongozo na auweke mrunda huo kwenye pembeya kitalu.Uwekaji wa alama unapaswa kufanyika kila mwaka kabla ya uvunaji kuanza. Vitalu vile tu ambavyo vitavunwa ndo viwekewe alama.

## 4. Mipaka ya Uvunaji


Sio miti yote iliyoko kwenye kitalu cha uvunaji inapaswa kukatwa. Mti wowote uliokondani ya mita 50 mwa kingo ya eneo dogo la usimamizi haupaswi kukatwa, ili mpaka wa eneo dogo la usimamizi wa msitu uonekane na usichanganywe na kilimo.

Miti yoyote katika eneo lenye mwinamo wenye kiwango cha asilimia 40 haupaswi kuvunwa pia (angalia mchoro 3). Eneo dogo la usimamizi kwa ajili ya mkaa linapaswa kuanzishwa kwenye maeneo ambao yana kiwango cha mteremko kilicho chini ya asilimia 40. Hata hivyo, unaweza kukuta maeneo madogo ndani ya eneo dogo la usimamizi ambayo yana mteremko mkali zaidi ya asilimia 40 na maeneo haya hayapaswi kuvunwa  kutokana nauwezekano kwa mmomonyoko wa udongo na usalama wachoma mkaa.

Ukataji wa miti karibu na vyanzo vya maji au makorongo unapaswa kudhibitiwa.  Hakuna miti inapaswa kukatwa ndani ya mita 15 ya kingo ya mto au vijito au korongo.




*Mchoro 3: Hatua za kutatuta mwinamo wa kitalu cha kuvuna miti*




*Mchoro 4: Miti ya mbao lakini haina sifa ya kupasuliwa mbao hutumika kwa kutengenezea mkaa*




Zaidi ya maeneo yaliyoainishwa kwa ajili yakutokatwa, pia kuna baadhi ya miti ndani ya vitalu vya uvunaji ambayo haipaswi kuvunwa kwa ajili ya mkaa.

➢ Miti iliyowekewa alama kwenye pembe za maeneo ya uvunaji wa mita 50 kwa 50 haipaswi kukatwa.

➢ Mti ambao una kipenyo cha chini ya sentimita 10 haupaswi kukatwa. Wachoma mkaa wanapaswa kupewa kifaa rahisi cha mbao cha kupimia vipenyo vya miti na kuweza kuainisha miti yenye kipenyo chini ya sentimita 10.

➢ Miti yenye thamani ya juu ya mbao yenye saizi yoyote ile haipaswi kukatwa kwa ajili ya utengenezaji wa mkaa labda kama imeumbika vibaya sana na haifai kwa mbao (angalia mchoro 4).




*Mchoro 5: Miti inayohifadhi bioanwai kama vile wanyama, ndege, haivunwi kwa ajili ya mkaa*

- Mti ambao una matumizi zaidi ya mawili, ambao una ukubwa zaidi ya sentimita 45 haupaswi kukatwa kwa ajili ya kutengeneza mkaa labda kama miti hiyo imeumbika vibaya sana na haifai kwa matumizi ya kuchana mbao (angalia mchoro 4)

- Miti ambayo ina viota vya ndege, makundi ya nyuki, au mapango madogo zaidi ya mita 3 haipaswi kukatwa. Miti aina hii ni makazi ya wanyama wadogo (angalia mchoro 5).

Kamati ya Maliasili ya Kijiji inapaswa kushirikiana na Afisa Misitu wa Wilaya, Meneja wa Misitu Wilaya kutoka Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania, na wazalishaji wa mbao ili kutengeneza orodha ya aina ya miti ya mbao yenye thamani ya juu na yenye matumizi zaidi ya mawili. Aina ya miti ya mbao itakayoainishwa kama yenye thamani ya juu, itahifadhiwa kwa ajili ya uzalishaji wa mbao tu - hata kama iko kwenye eneo la usimamizi na uzalishaji wa mkaa endelevu kama ni miti midogo sana kwa ajili ya mbao. Sababu kuu ni kuhakikisha kwamba miti ambayo inaweza kuletea faida zaidi kwa kijiji kama ikivunwa kwa ajili ya mbao haiharibiwi na kugeuzwa kwa kukatwa na kuchomwa mkaa ambao una thamani ndogo kuliko mbao.

**Kila mara uache angala miti mitatu ambayo kwenye kitalu cha uvunaji.**

Kama kitalu kilichopangwa kuvunwa kina miti michache chini ya miti mitatu ya mbao na makazi ya wanyama, ambayo haitokatwa, miti mingine ya ziada yenye kipenyo cha kati ya sentimita 10 hadi 30 inapaswa kuachwa ili ndani ya kitalu kimoja kunakuwa na angalau miti yenye ukubwa wa kati ambayo haijakatwa. Kamati ya Maliasili inapaswa kupanga kuacha miti mitatu ambayo haitokatwa ambayo imetawanyika vizuri katika kitalu kuliko kuwa na mkusanyiko wa miti katika eneo moja ya kitalu au miti pembeni mwa kitalu.





## 5. Miti ya mbao inayopaswa kuvunwa

Kimsingi, kijiji kinapaswa kuwa kilishakamilisha tathmini ya kiasi cha miti ya mbao kwa eneo lote la msitu wa hifadhi ya kijiji chao, wanapopanga kuvuna miti kwa ajili ya mbao, kabla ya kuanza kuvuna miti ya mbao kwenye maeneo madogo ya usimamizi mahsusi kwa mkaa. Kiwango cha mbao kinachopaswa kuvunwa kutoka kwenye maeneo madogo ya usimamizi kwa ajili ya mkaa katika mwaka mmoja hakipaswi kuzidi makadirio ya kiwango endelevu cha mbao kutoka kwenye eneo la usimamizi mdogo wa mkaa.

Mti kwa ajili ya mbao tu kwenye kitalu kinachopaswa kuvunwa iliyowekewa alama ndiyo inapaswa kuvunwa na pale tu kama ina kipenyo sawa au zaidi ya sentimita 45(ukitoa mti aina ya mpingo, ambao unaweza kuvunwa ikiwa na kipenyo cha sentimita 24 au zaidi). Miti ya mbao mikubwa kwa ajili ya kuvnwa inapaswa kukatwa ndani ya mwaka huo ambao kitalu cha mkaa kimevunwa kwa ajili ya mkaa. Haipaswi kujumuishwa katika hesabu za miti ya kukatwa katika kitalu kama inapaswa kuvunwa mwaka huo.

## 6. Rangi za kuwekea Alama miti

Kila Kamati ya Maliasili ya Kijiji inapaswa kuwa na aina za rangi zifuatazo kwa ajili ya kuweka alama wanapoenda kuweka alama kwenye kitalu cha uvunaji. Ni rahisi zaidi kufanya kazi na rangi ya kupuliza.

Rangi nyekundu – ni kwa ajili ya kuweka alama kwenye miti iliyoko kwenye pembe zote 4 za kitalu

Rangi ya chungwa – Kwa ajili ya kuweka alama miti ya makazi ya wanyama, miti ya mbao ambayo ni midogo sana kuchana mbao, na mipaka ya maeneo ambayo hayapaswi kukatwa miti kutokana na sababu kwamba ni maeneo yenye mteremko mkali, chanzo cha maji au korongo.


Rangi ya blu – Kwa ajili ya kuweka alama miti itakayokatwa kwa ajili ya mbao

Rangi ya njano –Kwa ajili ya miti ambao ina maumbile mabaya na haifai kuchana mbao bali inaweza kutumika kwa kuchoma mkaa.

Rangi nyeusi – Ni kwa ajili ya kuweka alama kwenye miti iliyokosewa rangi

Miti ambayo haijawekewa alama yoyote katika kitalu cha uvunaji na ambayo haiko ndani ya mita 15 ya chanzo cha maji, korongo au mteremko inadhaniwa kuwa inafaa kwa ajili ya kutengeneza mkaa.

Kila mti uliowekewa alama unapaswa kuwa na alama mbili. Alama ya mduara kuzunguka mti usawa wa urefu wa macho na mduara mzunguko chini kwenye mti (angalia mchoro 6).




*Mchoro 6: Alama za mwongozo wa uvunaji miti ya mkaa*



## 7. Hatua za Uvunaji

Kabla ya kutoa kibali kwa mchomaji mkaa, Kamati ya Maliasili lazima ihakikishe kwamba;

➢ Mchoma mkaa ni mwanachama wa umoja wa wachoma mkaa kijijini. Kwa kawaida umoja huu husajiliwa katika ofisi ya Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) ya wilaya kama wafanyabiashara wa mazao ya misitu kwa mwaka husika. Hii itathibitishwa kwa kuonyesha vielelezo sahihi.

➢ Kamati itampatia fomu ya maombi atakayotakiwa kuijaza kwa ukamilifu ikiwa na taarifa zote muhimu ikiwemo idadi ya magunia ya mkaa anayotaka kuchoma.

➢ Baada ya hapo Kamati itajadili maombi yake na kuyapitisha kulingana na vigezo vilivyowekwa. Moja ya sharti muhimu ni mwombaji kupata mafunzo ya uvunaji na uchomaji endelevu wa mkaa. Elimu hii hutolewa na wajumbe wa Kamati ya Maliasili ya Kijiji waliopatiwa mafunzo au wachomaji waliosajiliwa katika vikundi na kutambulika na Kamati ya Maliasili ya Kijiji.

➢ Kamati ya Maliasili ya Kijiji ni lazima ihakikishe kwamba mchomaji analipia leseni ya uvunaji kulingana na idadi ya magunia aliyoomba.

➢ Kamati ya Maliasili ya Kijiji itatoa kibali cha kumruhusu mchoma mkaa kuingia msituni endapo tu mchoma mkaa atakamilisha malipo yanayotakiwa kufanyika kwa serikali ya kijiji. Kibali hicho kitaainisha kipindi maalumu atakachokaa msituni, eneo atakalofanya uvunaji na idadi ya magunia atakayo choma.

➢ Kamati ya Maliasili ya Kijiji itachagua wajumbe wasiozidi wawili kwenda kumwonyesha mchoma mkaa eneo lililotengwa kuchoma mkaa ambalo litaweza kukidhi mahitaji ya mwombaji. Pia atamwonyesha miti inayofaa kwa mkaa na miti isiyo faa kwa mkaa. Miti isiyo faa kukata mkaa itakuwa na alama maalumu zilizowekwa na Kamati ya Maliasili ya Kijiji.

- Kamati ya Maliasili ya Kijiji itahakikisha kwamba sheria na taratibu zote zinazingatiwa wakati wote wa uchomaji wa mkaa ndani ya eneo dogo lililotengwa kwa uvunaji na kitalu husika.

## 8. Kuweka Kumbukumbu za takwimu

Pale ambapo kitalu cha kuvunwa kimewekewa alama, idadi ya miti inayofaa kwa ajili ya ktengeneza mkaa (siyo kwenye maeneo ambayo hayapaswi kuvunwa) inapaswa kuwekewa kumbukumbu ya ukubwa, kiwango katika kitabu maalum (angalia Jedwali 1).

Pia kila aina ya mti wa mbao (sio kwenye maeneo ambayo hayapaswi kuvunwa) inapaswa kuwekewa kumbukumbu na kufuatiliwa kwa ukubwa na aina.

Baada ya kuvuna, kumbukumbu hizi zinapaswa kurekebishwa zikionyesha idadi ya miti iliyobaki na idadi ya magunia ya mkaa yaliyozalishwa ikiwa ni pamoja na kiasi cha ushuru kilicholipwa kwa kijiji.

Kwa kuongezea, ili kusaidia kufuatilia uvunaji na mapato yanayotoka kwenye eneo dogo la usimamizi, kumbukumbu zinazowekwa zinaweza kutumika kubashiri wapi miti ya mbao inaweza kupatikana siku za usoni.







## Jedwali 1: Fomu ya Kumbukumbu za Kitalu

| Namba ya Utambulisho wa Kitalu #: | | Jira za longitudo: | | | | | | Jira za latitudo: | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ilichobakia (kipimo cha ukubwa) | | | | | | Iliyovunywa (kipimo cha ukubwa) | | | | | Ujazo/ Magunia yaliyozalishwa | Ushuru |
| Mwaka | Aina ya mti | 10-20 | 20-30 | 30-40 | 40-50 | 50-60 | > 60 | 10-20 | 20-30 | 30-40 | 40-50 | > 50 | | |
| 2015 | Miti ya Mkaa | | | | | | | | | | | | | |
| 2015 | Mtondoro | | | | | | | | | | | | | |
| 2015 | Msani | | | | | | | | | | | | | |
| 2015 | Mpingo | | | | | | | | | | | | | |
| 2015 | Mnyenye | | | | | | | | | | | | | |
| 2015 | Msolo | | | | | | | | | | | | | |
| 2015 | Mwanga | | | | | | | | | | | | | |

Kiongozi hiki kimeandaliwa kama sehemu ya utekelezaji wa Mradi wa Kuleta Mageuzi katika Sekta ya mkaa Tanzania.

**Lengo kuu:** Kuboresha namna ya kukabiliana na kuhimili mabadiliko ya tabia nchi; kuogeza uendelevu wa mazingira na kuongeza matokeo ya huduma za rasilimali za misitu; hivyo kuleta maendeleo endelevu kwa watu wa Tanzania.

**Dhumuni:** Kuanzisha mlolongo wa thamani wenye tija kibiashara kwa ajili mkaa unaozalishwa kwa njia endelevu kisheria.

**Kusudi:** Kuthibitisha njia bora zinazozingatia kuboresha umaskini za kupunguza ukatatiji wa miti hovyo na uharibifu wa misitu kwa kuleta mabadiliko katika sekta ya mkaa nchini Tanzania kwa kuanzisha masoko na mlolongo wa upatikanaji wa mkaa endelevu kama ukiongeza kuboresha usimamizi wa ujuzi na utawala bora katika sekta ya nishati hai.

Mradi huu unatekelezwa kwa ubia baina ya TFCG, MJUMITA na TaTEDO. Mradi huu ulizinduliwa rasmi mwaka 2012 na unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo na Ushirikiano la nchi ya Uswisi (SDC).